



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA ZA WATENDAJI WA**  
**VITUO VYA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA**  
**WAPIGA KURA**

Kwa madhumuni ya uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7 (4) cha Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 Mkurugenzi wa Uchaguzi anakaribisha maombi kutoka kwa watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi za **waandishi wasaidizi na waendeshaaji wa vifaa vya bayometriki**.

**A. SIFA ZA MWOMBAJI WA NAFASI YA MWANDISHI MSAIDIZI**

- (a) awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au zaidi na anajua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza;
- (c) awe mwenye ujuzi wa kutumia kompyuta au simu janja (Smartphone);
- (d) awe ni mkazi wa mtaa au kijiji katika kata anayoomba kuwa mwandishi msaidizi;
- (e) asiwe kiongozi au kada wa chama cha siasa; na
- (f) awe ni mwadilifu na mtiifu.

**B. SIFA ZA MWOMBAJI WA NAFASI YA MWENDESHAJI WA VIFAA VYA BAYOMETRIKI**

- (a) awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) awe amehitimu elimu ya kidato cha nne au zaidi na anajua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza;
- (c) awe mwenye ujuzi wa kutumia kompyuta au simu janja (Smartphone);
- (d) awe ni mkazi wa mtaa au kijiji katika kata anayoomba kuwa mwendeshaaji wa kifaa cha bayometriki;
- (e) asiwe kiongozi au kada wa chama cha siasa; na
- (f) awe ni mwadilifu na mtiifu.

### **C. MALIPO**

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo: -

- i. Kwa siku za uboreshaji wa Daftari vituoni waandishi wasaidizi na waendesaji wa vifaa vya bayometriki watalipwa posho ya Shilingi 50,000/= kwa siku na nauli Shilingi 10,000/=.
- ii. Wakati wa mafunzo, waandishi wasaidizi na waendesaji wa vifaa vya bayometriki watalipwa posho ya Shilingi 50,000/= na nauli Shilingi 10,000/= kwa kila siku ya mafunzo.

### **D. MASHARTI YA JUMLA**

- i. Mwombaji lazima aainishe nafasi anayoomba pamoja na kata anayoomba kufanyia kazi.
- ii. Mwombaji aambatishe: -
  - a. nakala ya vyeti vya Elimu ya Sekondari na Taaluma vinavyohitajika kulingana na kada husika kama vilivyofafanuliwa katika Tangazo hili.
  - b. wasifu (CV) ukionesha anuani yake ya makazi, namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini wake wawili.
  - c. picha mbili zenye ukubwa sawa na picha iliyomo kwenye pasi ya kusafiria (Passport size) za hivi karibuni.
  - d. barua ya utambulisho kutoka kwa mtendaji wa serikali ya mtaa au kijiji katika eneo analoishi.
- iii. Mwombaji ambaye ni mtumishi wa umma apitishe barua yake ya maombi kwa mwajiri wake.

**MWOMBAJI ATAKAYEBAINIKA KUWASILISHA TAARIFA ZA KUGHUSHI ATACHUKULIWA HATUA ZA KISHERIA.**



Barua zote za maombi ziandikwe kwa anuani ifuatayo: -

Mkurugenzi wa Uchaguzi,  
Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi,  
Uchaguzi House,  
Eneo la Uwekezaji Njedengwa,  
Kitalu D, Kiwanja Na.4,  
5 Barabara ya Uchaguzi,  
S.L.P. 358,  
**41107 DODOMA.**

**ILI KURAHISISHA UTUMAJI WA MAOMBI, BARUA ZOTE ZIKIWA  
ZIMEFUNGWA ZIPELEKWE KWA MTENDAJI WA KATA AMBAYE  
ATAZIPOKEA NA KUZIWASILISHA KWA MKURUGENZI WA  
HALMASHAURI**

**MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI NI TAREHE 27 APRILI, 2024**

Limetolewa na: -

  
Kailima, R.K.

MKURUGENZI WA UCHAGUZI  
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**DODOMA.**

15 APRILI, 2024



